**<u>TEGA SIKIO UJUFUNZE: EPISODE 4</u>**

# Ni vipi ujumbe mfupi wa simu ya rununu unaweza kumfikia Rafiki yako?

***Mwandishi: Lydia Heller***
***Mwelekezi: Maja Dreyer***
***Tafsiri : Anne Thomas/Eric Ponda***

***Mtangazaji***

***Jenny (15)***
***Jack (14)***
***Miriam, Rafikie Jenny (15)***
***Tom, Kakake Jack (18)***

## ***<u>Sehemu husika</u>***

***Chumbani kwa Jenny***
***Mahala nje, barabarani, katika bustani***
***Nyumbani kwa Jenny***

## *<u>Mazingira~ Sauti</u>*

Mtu akikoroga chai
Kurasa za gazeti zikipekuliwa
Sauti ya Jenny na Maria wakinongonezeana na kucheka
Simu ikipokea ujumbe mfupi
Mito ikikukutwa
Mlango ukifungwa kwa fujo
Mtu akitembea (akikaribia)
“ “ (akitokomea )
Pikipiki ikipita.
Mbinja
Pikipiki ikikaribia na kasha kuzimwa
“ “ ikiwashwa.
Mlango ukibishwa
Mlango ukifunguliwa taratibu
Mtu akibofya kizenji cha simu ya mkononi
Mtu akichukua simu kutoka mezani

***INTRO(Mtangazaji):***

Hujambo na karibu kwa mfululizo wa mchezo wetu wa Redio, Tega sikio ijifunze, unaozungumzia mambo ambayo huchukuliwa ya kawaida na bila ya kujishuhghulisha kujua jinsi yanavyotendeka na kwanini..

Kwa mfano, vipi simu ya mkononi inavyofanya kazi.Au ni vipi mtu anavyoweza kupokea au kutuma ujumbe mfupi kwa kutumia simu ya mkononi au rununu?

Jack anatumia simu yake mpya ya mkono kumtumia ujumbe Jenny kumtaka wakutane mahali.Lakini kwabahati mbaya siri inafichuka kwani ujumbe huu unamfikia Miriam kimakosa badala ya Jenny.Mariam anapokea ujumbe akiwa nyumbani pamoja na Jenny.

***Sura ya Kwanza***

**Jenny na rafikiye Miriam wameketi wakipiga gumzo huku wakinongonezeana na kucheka. Ghafla Miriam anapokea ujumbe kwenye simu yake ya mkononi..Jambo hilo linamkasirisha Jenny**.

*(Sauti ya Mtu akikoroga Chai kikombeni, kurasa za gazeti zikipekuliwa huku huku Jenny na Miriam wakisikika wakiongea,kunongonezana na kucheka).*

*(simu ikipokea ujumbe mfupi..)*

**Miriam:** Aha, hiyo ni simu yangu *(akiwa na hamaki)*.Ni ujumbe!.(*akishangaa unakotoka ujumbe huo)*
Sijui nani kanitumia ujumbe huu.

**Jenny:** *(akimtania rafikiye)*¡°Oooooh rafiki yangu Miriam amepokea ujumbe*!(anacheka)* Kuna mtu anayekuhusudu! Mambo haya ni gharama!(anacheka huku akimgusa-gusa)Bila shaka
unatoka kwa Daniel-yule mvulanamtundu! Amekuwa akikunyemelea kwa muda sasa! *(Kwa hamu kubwa)* nionyeshe basi!

**Miriam:** *(akisoma ujumbe huku maneno yakimsakama)*Tuneweza kuonana kesho baada ya masomo?

***Miriam na Jenny kwa pamoja…..***tayari roho yanidunda! *(wakiiongea kwa sauti,ingawa Miriam bado anashaka na ujumbe huu huku Jenny akiungulika moyoni***)….*** wako Jack!

Miriam: *(akiwa amechanganyikiwa, lakini furaha moyoni)*Kutoka kwa Jack!

**Jenny:** (*akiwa amechanganyikiwa )* Kutoka kwa Jack!

**Miriam:** Ameandika "Ni wako Jack"!Na anataka tukutane baada ya shule!

**Jenny:** *(kwa hasira)* Lakini hutaenda kumuona, au?

**Miriam:** *(akimkatiza)*Kwa nini nisiende?

**Jenny:** *(akiwa na hasira huku akijaribu kutafutasababu)*Kwa sababu….. aah kwa sababu Jack ni mjinga sana.Anapenda kujionyesha. Namjua toka tukicheza naye kandanda.--- ana mdomo, kila wakati kujigamba tu.

**Miriam:** *(amkatiza Jenny kwa madaha)*Aaah, waona.. wivu huo!

*(Sauti ya mito ikikukutwa na hatua za haraka)*

**Miriam:** Aii Jenny, umekasirika *( huku akimwita)*…..Usiende ni mzaha tu! Kwani waendapi? Tena na simu yangu?

*(Mlango wafungwa kwa kishindo…..)*

**Muziki….**

**<u>SURA YA PILI.</u>**

Jenny anamkabili Jack na ule ujumbe katika simu ya Miriam- ujumbe ambao Jack alinuia kumtumia Jenny.

(***Sauti ya hatua za haraka zikikaribia***.)

**Jack:** (*akiwa na furaha japo na mshangao)* Aa¡Jenny, hujambo?

**Jack:** *(akiwa amechanganyikiwa kidogo*) Jenny? Nini mbaya?

**Jenny:** *( akiwa amekasirika )*Nikusomee ujumbe hapa Jack?

**Jack:** *(bado amechanganyikiwa*)Bila shaka, soma!

Jenny: *( akisoma kwa sauti ya juu, kirasmi,lakini bila raha)*
"Twaweza kukutana kesho baada ya shule? Tayari roho yanidunda….wako Jack!!".

**Jack:** *(akiona haya, tayari ametambua ujumbe alioutuma wa na anataka kujua ikiwa Jenny atakubal)*
Si ndio. Na Sasa wasemaje?

**Jenny:** *(kwa ghadhabu)* ATI NASEMAJE….MIMI? Wacha mzaha! Hebu niambie ujumbe huu ulifikaje kwa simu ya Miriam?

**SURA YA 3 : Jack anakutana na kakake anayemueleza jinsi ujumbe unavyoweza kumwendea Mtu asiyekusudiwa --- Jack aona raha,**

( *Hatua za haraka zikitokomea).*

**Jack:** *(sauti ya juu)*Jenny, subiri kidogo. Sikukusudia hivyo.*( huku akiongea pekee,pole pole)* Sijui ilikuaje!. Ilikuaje hata ujumbe huo ukamwendea Miriam? Kwa kweli ni upumbavu wangu.

***(Mlio wa pikipiki ikipita kisha  mbinja***.)

**Tom:** *(sauti kutoka kwa hiyo pikipiki)* Wee, Jack!

**Jack:** *( akiongea pekee huku akijilaumu*) Balaa gani tena hii --- kakangu, bahati mbaya ilioje!

**Tom:** *(kwa sauti ya juu)* Jack? Kwani siku hizi umekuwa kiziwi, au vipi?

***(Mlio wa pikipiki ukikaribia, halafu unazima).***

**Tom:** Kulikoni ndugu? Tutaandamana? Tunaenda kuogelea na marafiki zangu kadha, tutawababaisha wasichana --- katika ile hali ya kuwachemsha tu!

**Jack:** *(akiwa na hasira)* La hasha, sina haja ya kuwaudhi mamanzi

**Tom:** Unasumbuliwa na nini, ndugu, waonekana kama ambaye mama amekupa kazi ya wiki tatu. Nini mbaya? *(huku akimtania)* Kaka wasichana wanakusumbua nini?

**Jack:** *(kwa hasira)* Nyamaza wewe! Kusumbuliwa na wasichana! Wacha upuzi!

**Tom:** *(akitambua ukweli)* Kwa hivyo unayo matatizo ya wasichana! Hebu, katika kubahatisha tu. Ulimwalika yule Jenny wa darasa la saba mwende mkanywe soda, akakataa, sio?

**Jack:** *(Atamka kwa haraka)* LA HASHA! *(amegunduliwa)* Nani azungumza kuhusu Jenny.?

**Tom:** *(akiwa amejua ukweli,akimtania Jack)* Sawa, sawaa, naelewa. Huna haja na Jenny. Kwa kweli mimi humuona kama ni mbumbumbu yule.

Jack: *(akiudhika zaidi)* NINI ? Usithubutu, tena

ukome kusema hivyo. Jenny si *(maneno yamkwama, ajua siri yake imegunduliwa)*

**Tom:** *(huku akitabasamu)* Eehe?

**Jack:** *(akikubali ukweli, anapumua kwa nguvu)* Ndio nilimtumia Jenny ujumbe na simu yangu mpya ya mkono leo asubuhi, nikitaka tukutane kesho baada ya shule. Lakini ajabu ni kwamba ujumbe huo umepokewa na simu ya Mtu asiyekusudiwa!.

**Tom:** Unamaanisha nini, simu ya Mtu mwengine?

**Jack:** Ujumbe ulikwenda katika simu ya Miriam, swaibu mkubwa wa Jenny!.

**Tom:** *(akipiga mbinja)* Uuuuuwi¡..wasichana kamwe hawapendelei mambo hayo *(kama mjuzi wa mambo)*Ni limbukeni wa mambo ya teknolojia. Labda ulibonyeza makosa kibonyezi na ukaenda kwa nambari usiyokusudia!

**Jack:** Kabisa! Hivyo ndivyo ilivyokuwa! (*kwa sauti ya chini kidogo)* Hata hivyo sitasema ujinga niliofanya kubonyeza nambari isiyo. *(sasa kwa majivuno)* Kakangu umebobea katika mambo haya ya risala za simu za mkono! kwa kweli umenisaidia sana!

***(Sauti ya pikipiki ikiwashwa)***

**Jack:** *(kwa ukulele)* Haraka ndugu. Sharti tumfikie Jenny upesi iwezekanavyo!

**Muziki…..** *( kwa ufupi)*

## <u>SURA YA 4.</u>

**Mwisho: Jack amweleza Jenny jinsi ujumbe wa simu ya mkono unavyotoka kwenye simu moja hadi nyingine.**

.(*Mlio wa kubishwa kwa mlango)*

**Jack:** Jenny, tafadhali fungua mlango¡ ni mimi
Jack. Sasa nimejua kilichotendeka, nitakueleza!.

*(Mlango wafunguliwa taratibu)*

**Jenny:** *(bado hana raha, lakini mdaku)* Sawa,
nakusikiliza, niambie!.

**Jack:** Chukulia simu za mikono na jumbe zake,kama mimi na wewe na mama zetu.

**Jenny:** *(akimkatiza)* Usimhusishe mamangu katika mambo
Haya. Kamwe hahusiki na mambo haya ya upuzi.

**Jack:** *(akijifanya hakusikia)* Ooooh Jenny! Tafadhali nisikilize. Yaani mimi na wewe ni kama simu za mkono. Kila simu ya mkono imesajiliwa na kampuni inayoitolea huduma kupitia mtandao unaohakikisha kwamba simu za mkono zinafanya kazi. Unaona!, ni kama mama zetu. Na daima hizi kampuni zinazotoa huduma hujua kila simu yao iko mahali gaini.

**Jenny:** *(akionekana kushawishika)* Kwa hivyo simu hizi
hueleza hizo kampuni hizo mara kwa mara kule ziliko, kama vile ninavyo mwambaia mamangu ninakokwenda?

**Jack:** Hasa.Wakati mtu anapoandika ujumbe kwenye simu ya mkono, ujumbe huo kwanza huenda kwa kampuni yamtandao inayomhudumia.Kisha kwa nambari ambayo
imehifadhiwa kwenye simu hiyo. Halafu kituo cha
kusambaza jumbe hizo hutoa habari kuhusu mahali ilipo simu inayopelekewa ujumbe na kampuni ya mtandao inayoihudumia. Ndipo hapo kituo hicho cha kusambaza risala kinawasilisha risala hiyo kwa kampuni ya mtandao husika, ambayo nayo huwasilisha risala
hiyo kwa simu inayokusudiwa

**Jenny:** Yaani simu ya mkono kwa mfano Jenny anaujumbe wa rafiki

simu ya Mkono tuseme Jack, na simu ya mkono Jack inamwambia

mamake, yaani kampuni ya mtandao. Simu ya mkono Jenny haijui simu

ya mkono Jack iko wapi.

Lakini simu ya mkono Jenny inajua kwamba kampuni yake ya mtandao

ambayo ni mamake tunasema ni mamake inajuana na kampuni ya pili ya

mtandao ambayo tunasema ni mamake Jack kwani hukutana mara kwa

mara katika soko la kijijini na kuzungumza. Na hivyo basi kama kina

mama mtandao, wanajua watoto wao, ambao ni zile simu za

mkono, wako wapi.Kampuni ya mtandao mamake Jenny inajua inapaswa kuwasilisha risala kwa simu ya mkono Jack na inatoa risala hiyo kwa kampuni ya mtandao-mamake Jack. Papo hapo mamake Jack inatafuta simu ya mkono Jack na kuwasilisha risala hiyo.

**Jack:** *(akicheka)* Kabisa. Ndivyo hivyo

**Jenny:** (*kwa uzuri)* Ni ajabu *(kisha ghafla akasirika)* hata hivyo sielewi kwa nini kampuni mtandao mamake Jack iliwasilisha ujumbe wako kwa simu ya mkono MIRIAM!

**Jack:** *(akiwa amechanganyikiwa)* Kampuni ya Mtandao hutafuta na kutuma ujumbe unakokusudiwa kutoka kwa ile orodha ya anwani zilizoko. Hivyo basi huenda kampuni hiyo, mamake Jack ilielewa vibaya na kutuma ujumbe kimakosa… aaah balaa gani hii!. Ukweli ni kwamba nilibonyeza nambari kwa makosa! Lakini nitakutumia tena risala hiyo sasa hivi. Subiri.

*(Mlio wa vibonyezi vya simu unasikika)*

Jack: Nishautuma. Kwisha!. Subiri kidogo tu!.

*(.Mlio wa simu: ikipokea risala ya maandishi).*

**Jack:** Ndiyo hiyo risala imwasili. Hebu nikusomee.

*(Anachukua simu kutoka mezani.)*

**Jack:** *( huku akiwa na mchecheto)* Mpendwa Jenny!
Twaweza kukutana kesho baada ya shule? *(kwa utaratibu zaidi, na mshangao)* Nakusubiri, ni mimi wako
*(akimuulizo na hasira)* DANIEL?????

**Muziki…**

---

OUTRO

(Mtangazaji) Bahati mbaya kwa Jack.Imebainika kwamba risala ya mpinzani wake, Daniel imewasili kwanza kwenye simu ya Jenny, na yuataka kukutana naye baada ya shule.

Lakini swali ni Je,Daniel ana ujuzi unaostahili wa kutuma risala za maandishi kwa simu ya mkono kama Jack?
Na je, anajua kikamilifu jinsi teknolojia hii inavyofanya kazi.
Kuna maswali mengi tu kuhusu maisha yetu ya kila siku ambayo huchukuliwa kuwa mambo ya kawaida ingawa hakuna mtu anayejua majibu yake? Ni Mengi!.
Mchezo wa le TEGA SIKIO UJIFUNE umeandikwa na Lyidia Heller.
Pia unaweza kutusikiliza kupitia mtandao wetu
www.dw.de/kiswahili. Asante kwa kutusikiliza na
Hadi wakati mwengine kwa makala nyingine Kwaheri..